

Maswali

1. Paulo alienda mji gani kufundisha juu ya Yesu?
2. Nani alienda na Paulo?
3. Mbona Paulo hakupenda yule kijakazi kuwafuata?
4. Paulo alifanyaje yule kijakazi.
5. Mbona wenye yule msichana waliwapeleka Paulo na Sila kwa waamuzi?
6. Nini ilifanyika kwa Paulo na Sila?
7. Paulo na Sila walifanya nini usiku wa manane?
8. Nini ilifanyika usiku wa manane?
9. Mbona mlinzi wa gereza aliogopa?
10. Paulo aliambia mlinzi afanye nini ili aokoke?

Majibu

1. Paulo alienda Filipi kufundisha juu ya Yesu.
2. Sila alienda na Paulo.
3. Kijakazi aliendelea kuwapigia kelele kwa sababu hakukuwa na akili mzuri.
4. Paulo alimponya yule kijakazi.
5. Walikasirika kwa sababu hawangepata pesa baada ya yule msichana kuponywa tena hangeweza kuwambia maneno yao yajayo.
6. Walipigwa, wakawekwa gerezani na miguu yao ikafungwa na mkatale.
7. Waliimba nyimbo na kuomba Mungu.
8. Kulikuwa na tetemeko ya nchi, milango ya gereza ikafunguka na minyororo za wafungwa zikalegea.
9. Alifikiria kwamba wafungwa wote walikuwa wamatoroka.
10. Paulo aliambia mlinzi aamini na abatizwe.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



50 Paulo na Sila gerezani

Marejeo

Matendo ya Mitume 16: 16 - 40

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Paulo na Sila waliamini na kumsifu Mungu hata kama walikuwa kwa shida


Maneno maalum

- 50.1 Paulo + fundisha juu ya Yesu + Sila + Filipi
- 50.2 Kijakazi + sema yajayo + fuata + piga kelele + Paulo + ponya + wenyewe + kasirika + waamuzi + uongo
- 50.3 Paulo + Sila + pigwa + gereza + mkatale + usiku wa manane + waliimba nyimbo + omba + Mungu alifurahi + tetemeko la nchi + milango ikafunguka + vifungo vikalegea
- 50.4 Mlinzi wa gereza + ogopa + fikiri wafungwa wamtoroka + usiogope + wote wako + Nifanye nini? + amini + batizwa + Paulo na Sila + wakaondoka gerezani

50.1 Paulo (jina lake lilibadilishwa kutoka kwa Sauli) alienda miji mingi akifundisha watu. Aliwafundisha juu ya Yesu na Ufalme waajabu wenye atakuja kusimamisha wakati akirudi hapa duniani. Siku moja alienda pamoja na rafiki yake Sila kwa mji wa Filipi. Paulo alienda kando kando ya mto akifundisha watu juu ya Yesu.

50.2 Huko Filipi kulikuwa na kijakazi. Alikuwa na ugonjwa wa akili. Aliambia watu ni nini ingefanyika kwao siku zijazo. Alitengezea watu wake pesa nyingi sana. Huyu kijakazi aliendelea kumfuata Paulo na Sila akipiga kelele. Paulo hakupenda huyu msichana kuwapigia kelele. Kwa hivyo, siku moja Paulo akamponya kwa jina la Yesu.

Huyo kijakazi alipoona, hangeweza kuambia watu mambo yao ya siku zijazo. Watu wake walikasirika sana kuona kwamba amepona. Hangeweza kuwaletea pesa tena kwa sababu hakuwambia maneno yajayo. Walishika Paulo na Sila na kuwaburura mpaka sokoni. Waliwapeleka mpaka mbele ya waamuzi. Walisema uongo juu ya Paulo na Sila.




50.3 Paulo na Sila walipigwa. Halafu wakapelekwa gerezani. Miguu yao ilifungwa kwa mkatale.

Kama tungekuwa kwa baridi, ndani ya gereza iliyo na giza, migongo ina vinonda vya kupigwa hali miguu yetu imefungwa kwa mkatale, nina ukweli tungejisikitikia sana. Lakini Paulo na Sila walikuwa na ujasiri sana. Walijua kwamba Yesu alikufa kwa ajili yao na ni vizuri nao waumia kwa ajili yake. Katikati ya usiku waliomba na kuimba nyimbo wakimsifu Mungu. Wafungwa wenzao walishangaa kuwaona hao wafungwa wawili waliokuwa wamepigwa wakiimba nyimbo.

Mungu alifurahi sana kuona vile Paulo na Sila walikuwa na ujasiri na akajibu maombi yao. Kwa ghafula kulikuwa na tetemeko kuu ya nchi. Gereza ilitikisika, milango yote ilifunguka na minyororo za wafungwa zililegea pia.

50.4 Mlinzi wa gereza aliogopa sana. Alifikiria kwamba wafungwa wote walikuwa wameteoroka. Paulo alipaza sauti, “Usiogope. Tuko hapa wote.” Mlinzi wa gereza alileta taa na akaja kuangalia. Alianguka chini ya miguu ya Paulo. Aliuliza, “Lazima nifanye nini ili nipate kuokoka?”



Paulo alimwambia, “Lazima uamini kwa Bwana wetu Yesu Kristo halafu utaokoka.” Paulo aliambia yule mlinzi wa gereza pamoja na familia yake juu Yesu. Wote waliamini na wakabatizwa. Usiku huo mlinzi aliwalinda Paulo na Sila na kesho yake waliachiliwa.